**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO**
**OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO**
S.L.P 3000, CHUO KIKUU, MOROGORO, TANZANIA.
Simu Na.: +255 (023) 2640006/7/8/9, Moja kwa moja:
+255 (023) 2640015,
Barua pepe: vc@sua.ac.tz, Tovuti: https://www.sua.ac.t

***Unapojibu tafadhali taja:***
**Kumb. Na.** EA.12/216/01/02 **Tarehe:** 27.08.2025

## TANGAZO LA AJIRA ZA MUDA KWA WAHITIMU HAMSINI (50) WENYE TAALUMA YA KILIMO KWA AJILI YA KUENDELEZA ZAO LA PARACHICHI

## UTANGULIZI

Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo (MoA) kinatekeleza programu ya kushirikisha vijana katika kilimo ya Jenga Kesho iliyo Bora katika mazao mbalimbali nchini. Katika mpango wa BBT- Parachichi, SUA na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko - COPRA imeandaa mpango wa kutumia wahitimu hamsini (50) wenye taaluma ya kilimo kwa kipindi cha miezi kumi na mbili (12) kutoa huduma za Ugani kwa ajili ya programu maalum ya kuendeleza zao la parachichi nchini. Mpango utatekelezwa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2025/2026 ikiwa ni maandalizi ya uzalishaji wa parachichi ghafi. Mpango huu utatekelezwa katika Wilaya ya Rugwe, Mkoa wa Mbeya.

Aidha, katika Utekelezaji wa program hii maalum ya huduma za ugani kupitia vijana wahitimu katika fani za kilimo (BBT Agricultural Extension Entrepreneurship Scheme - BBT AEES), inahitaji wahitimu hamsini (50) wenye sifa stahiki katika fani za kilimo ili kutoa huduma za ugani katika zao la parachichi kwa utaratibu wa ajira za muda kama ifuatavyo:-

1. **Nafasi: Afisa Kilimo/ (Nafasi 5)**
   ***Majukumu ya muhimu ni pamoja na:***
   (a) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa zao la parachichi kwa kufanya yafuatayo:-
      i. Kutoa elimu ya kilimo bora cha parachichi kwa wakulima kuanzia kuandaa shamba, kutunza shamba, kuvuna, kuongeza thamani, kuhifadhi hadi kuuza sokoni.
      ii. Kutoa elimu na kusimamia ubora wa parachichi ghafi kuanzia shambani hadi ghalani.
      iii. Kufuatilia na kuhakikisha wakulima wanazingatia Kanuni za kilimo bora cha parachichi.
      iv. Kuandaa na kutoa taarifa kila wiki kuhusu maendeleo ya kilimo cha parachichi katika eneo husika la kazi.
      v. Kuandaa mahitaji halisi ya pembejeo ikiwa ni pamoja na mbegu/miche kwa wakulima na kuwasilisha.
      vi. Kusimamia na kuhakikisha pembejeo zilizosambazwa katika eneo husika zinawafikia wakulima na wanazitumia katika mashamba yao ya miparachichi.
      vii. Kufanya tafiti ndogo shambani na majaribio ya kilimo ili kupima aina bora za mbegu, mbolea au teknolojia mpya.

(b) Kuhuisha kanzidata ya wakulima wa parachichi na wadau wengine ikiwemo watoa huduma za pembejeo katika eneo lake kwenye mfumo wa kidijitali uliopo.
(c) Kusimamia ugawaji wa pembejeo za ruzuku za zao la parachichi zinazotolewa na Serikali kwa wakulima wa parachichi katika eneo lake la kazi.
(d) Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha parachichi ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa wakulima.
(e) Kusimamia uhakiki wa ubora wa parachichi katika ngazi ya Chama cha Msingi cha Ushirika (AMCOS).
(f) Kuandaa makadirio ya uzalishaji wa parachichi ghafi kwa kuzingatia kigezo cha miti ya miparachichi iliyopo yenye uwezo wa kuzalisha katika msimu husika *(Crop forecast)*.
(g) Kuwatambua wadau wa sekta ya kilimo waliopo katika eneo husika la kazi na kuwaunganisha na wakulima ili kupata huduma wanazotoa.
(h) Kuhakikisha kila mkulima ana daftari ambalo litatumika kujaza huduma zitakazotolewa na wadau mbalimbali wakiwemo maafisa ugani kilimo.
(i) Kushirikiana na uongozi wa kijiji kuchagua mkulima kiongozi *(Lead farmer).*
(j) Kutoa ushauri kwa mazao mengine na yanayolimwa na wakulima wa Kijiji/eneo analosimamia.
(k) Kufanya tathmini ya uzalishaji wa parachichi katika eneo lake la kazi kila mwisho wa msimu na kuwasilisha taarifa.
(l) Kusimamia maafisa ugani wasaidizi katika eneo husika.
(m) Kufanya shughuli nyingine yoyote atakayopangiwa na kiongozi wake.

**Sifa zinazohitajika**

Kijana muhitimu wa fani ya kilimo ngazi ya shahada *(Degree)* mwenye sifa zifuatazo:-

i. Awe mtanzania mwaminifu, mwadilifu, mwenye kujituma na mahusiano mazuri na wengine.
ii. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 40.
iii. Awe amehitimu shahada *(Degree)* katika fani ya Sayansi ya Kilimo (Agriculture General), Agronomia (Agronomy), Kilimo cha Bustani (Horticulture) au Uzalishaji na Usimamizi wa Mazao (Crop Production) kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali.
iv. Asiwe ameajiriwa au kufukuzwa kazi katika utumishi wa umma.
v. Awe hajawahi kufungwa kwa makosa yoyote ya jinai.
vi. Awe tayari kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ya vijijini.
vii. Awe na uwezo wa kufanya kazi vizuri bila kusimamiwa.
viii. Awe tayari kufanya kazi kwa mkataba wa muda na kulipwa posho ya mwezi kama itakavyoainishwa katika mkataba.
ix. Awe tayari kusaini mkataba wa makubaliano wenye vigezo vya utendaji kazi kwa kipindi cha msimu husika.
x. Uzoefu wa kazi katika zao la parachichi ni sifa ya ziada.

2. **Nafasi : Afisa kilimo msaidizi (Nafasi 45)**
**Majukumu ya muhimu ni pamoja na:**

a) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa zao la parachichi kwa kufanya yafuatayo:-

   i. Kutoa elimu ya kilimo bora cha parachichi kwa wakulima kuanzia kuandaa shamba, kutunza shamba, kuvuna, kuongeza thamani, kuhifadhi hadi kuuza sokoni.
   ii. Kutoa elimu na kusimamia ubora wa parachichi ghafi kuanzia shambani hadi ghalani.
   iii. Kufuatilia na kuhakikisha wakulima wanazingatia Kanuni za kilimo bora cha parachichi.
   iv. Kuandaa na kutoa taarifa kila wiki kuhusu maendeleo ya kilimo cha parachichi katika eneo husika la kazi.
   v. Kuandaa mahitaji halisi ya pembejeo ikiwa ni pamoja na mbegu/miche kwa wakulima.
   vi. Kusimamia na kuhakikisha pembejeo zilizosambazwa katika eneo husika zinawafikia wakulima na wanazitumia katika mashamba yao ya miparachichi .

b) Kuhuisha kanzidata ya wakulima wa parachichi na wadau wengine ikiwemo watoa huduma za pembejeo katika eneo lake kwenye mfumo wa kidijitali uliopo.
c) Kusimamia ugawaji wa pembejeo za ruzuku za zao la parachichi zinazotolewa na Serikali kwa wakulima wa parachichi katika eneo lake la kazi.
d) Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha parachichi ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa wakulima.
e) Kusimamia uhakiki wa ubora wa parachichi katika ngazi ya Chama cha Msingi cha Ushirika (AMCOS).
f) Kuandaa makadirio ya uzalishaji wa parachichi ghafi kwa kuzingatia kigezo cha miti ya miparachichi iliyopo yenye uwezo wa kuzalisha katika msimu husika *(Crop forecast)*.
g) Kuwatambua wadau wa sekta ya kilimo waliopo katika eneo husika la kazi na kuwaunganisha na wakulima ili kupata huduma wanazotoa.
h) Kuhakikisha kila mkulima ana daftari ambalo litatumika kujaza huduma zitakazotolewa na wadau mbalimbali wakiwemo maafisa ugani kilimo.
i) Kushirikiana na uongozi wa kijiji kuchagua mkulima kiongozi *(Lead farmer).*
j) Kutoa ushauri kwa mazao mengine yanayolimwa na wakulima wa Kijiji/eneo analosimamia.
k) Kufanya tathmini ya uzalishaji wa parachichi katika eneo lake la kazi kila mwisho wa msimu
l) Kufanya shughuli nyingine yoyote atakayopangiwa na kiongozi wake.

**Sifa zinazohitajika**

Kijana muhitimu wa fani ya kilimo ngazi ya Stashahada *(Diploma)* mwenye sifa zifuatazo:-

i. Awe mtanzania mwaminifu, mwadilifu, mwenye kujituma na mahusiano mazuri na wengine.
ii. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 35.
iii. Awe amehitimu Stashahada *(Diploma)* katika fani ya Sayansi ya Kilimo (Agriculture General), Agronomia (Agronomy), Kilimo cha Bustani (Horticulture) au Uzalishaji na Usimamizi wa Mazao (Crop Production) kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali.
iv. Asiwe ameajiriwa au kufukuzwa kazi katika utumishi wa umma.
v. Awe hajawahi kufungwa kwa makosa yoyote ya jinai.
vi. Awe tayari kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ya vijijini.

vii. Awe na uwezo wa kufanya kazibila kusimamiwa.
viii. Awe tayari kufanya kazi kwa mkataba wa muda na kulipwa posho ya mwezi kama itakavyoainishwa katika mkataba.
ix. Awe tayari kusaini mkataba wa makubaliano wenye vigezo vya utendaji kazi kwa kipindi cha msimu husika.
x. Uzoefu wa kazi katika zao la parachichi ni sifa ya ziada.

**Namna ya kutuma maombi**

Maombi yote yaambatane na;

a) Vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, NIDA, vyeti vya elimu ya sekondari, stashahada na shahada kutoka vyuo vya mafunzo vinavyotambuliwa na serikali (viwe faili moja).
b) Picha mbili za hivi karibuni za “passport size” za mwombaji
c) Wasifu (Curriculum Vitae) wa mwombaji pamoja na anuani kamili, mawasiliano ya simu, barua pepe na anuani za wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

Maombi yote yatumwe kwa Rasi wa Ndaki ya Kilimo ya Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo kupitia barua pepe coahr@sua.ac.tz na nakala kwa Mkurugenzi, Kurugenzi ya Shahada za Awali ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo dus@sua.ac.tz. Waombaji wanashauriwa kutuma maombi yao kupitia barua pepe ingawa wanaweza pia kuleta maombi moja kwa moja kwa ofisi tajwa hapo juu au EMS.

**Mwisho wa kutuma Maombi**

Maombi yote yawe yametufikia kabla au ifikapo tarehe **12 Septemba 2025.**
Kwa maelezo zaidi au maswali juu ya tangazo hili tafadhali tupigie kupitia namba zifuatazo:
+255760485718

Limetolewa na
Makamu Mkuu wa Chuo
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Morogoro